

OFIS YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA
KANDA YA BUHARE MTHANI WA ROBO MUHULA APRILI 2025

KISWAHILI
KIDATO CHA TATU

MUDA: Saa 3:00

Maelekezo

- ❖ Karatasi hii ina sehemu **A, B na C** zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
 - ❖ Jibu maswali yote katika sehemu A na B, na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C.
 - ❖ Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
 - ❖ Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
-

SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali yote

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) – (x) na uandike herufi ya jibu katika kisanduku
 - i. Huyu ni mwanafunzi Hodari sana. Je, neno “ni” ni aina gani ya neno?
 - a) Kitenzi kishirikishi
 - b) Kiunganishi
 - c) Kitenzi kisaidizi
 - d) Kielezi cha wakati
 - ii. Njia ipi ya uhifadhi wa fasihi simulizi inayoweza kupokea mabadiliko kwa haraka kati ya hizi?
 - a) Maandishi
 - b) Vinasauti
 - c) Kichwa
 - d) Kanda za video
 - iii. Tofauti ndogondogo zinazojitokeza katika lugha moja huitwa.....
 - a) Kimtang’ata
 - b) Lugha za kikanda
 - c) Lahaja
 - d) Kiimbo
 - iv. Wazo kuu la mtunzi katika fasihi huitwa.....
 - a) Ujumbe

MsomiBora.com

- b) Dhamira
- c) Falsafa
- d) Mtazamo

v. ni maneno yasiyo sanifu yanayozuka na kutoweka

- a) Misimu
- b) Rejesta
- c) Misamiati
- d) Kishazi tegemezi

☐

vi. Kisawe cha neno “maskini” ni.....

- a) Ukwasi
- b) Ubahili
- c) Ijima
- d) Ukata

☐

vii. Neno pamoja na taarifa zake kwenye kamusi huitwa.....

- a) Kidahizo
- b) Kitomeo
- c) Msamiati
- d) Muundo

☐

viii. Utofauti wa kazi za kifasihi toka mwandishi mmoja dhidi ya mwingine husababishwa na.....

- a) Mtindo wa kazi
- b) Dhamira za kazi ya fasihi
- c) Migogoro ya kazi husika
- d) Muundo wa kazi husika

☐

ix. Moja ya sifa kuu ya Kirai ni.....

- a) Kukaa sehemu yoyote katika sentensi
- b) Hakina muundo wa kiima na kiarifu
- c) Hutoa maana kamili
- d) Huwa na muundo wa kiima na kiarifu

☐

x. Neno lipi kati ya maneno yafuatayo hudokeza zaidi juu ya mtenda au mtendwa wa jambo?

- a) Kiunganishi
- b) Kihisishi
- c) Kielezi
- d) Kivumishi

☐

2. Oanisha maana ya dhana zilizo katika orodha A kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika orodha B

ORODHA A	ORODHA B
i. Ngeli	A. Pangani, Asha, Usingizi na John
ii. Sentensi	B. Anayesinzia ni mvivu
iii. Nomino za pekee	C. Chaki
iv. Neno lenye mofimu nne	D. PAMUKU
v. Kiambishi cha nafsi ya pili wingi	E. <u>W</u> anaimbiwa
	F. <u>M</u> naimbiwa
	G. Mtoto
	H. Tunakula
	I. Kariakoo, Tanga, Iringa na Ali
	J. Wewe ni mvivu

ORODHA A	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)
ORODHA B					

SEHEMU B (Alama 55)

SARUFI, UTUMIZI WA LUGHA NA MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu maswali yote

3. Tunga sentensi au tungo kwa kila kipengele (*i – iv*) ukizingatia viambajengo vya kila kipengele.
 - i. Kishazi tegemezi + kishazi huru
 - ii. Kishazi huru
 - iii. Kishazi huru + kishazi huru
 - iv. Kishazi tegemezi
 - v. Kishazi tegemezi + kishazi tegemezi
4. Toa maana mbili za maneno yafuatayo:
 - i. Paa
 - ii. Mbuzi
 - iii. Kanga
 - iv. Tai
 - v. Kata
5. Katika sentensi zifuatazo, oneshwa matumizi ya mofimu “Ki”
 - i. Ukimuona atakueleza
 - ii. Alikuwa akilia gari lilipogonga mti
 - iii. Ameua kifalme

- iv. Kikombe kimevunjka
- v. Amechukua kimoja tu

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) katika sehemu hii

- 6. Jifanye wewe ni muhitimu wa kidato cha nne mwaka 2022 umeliona na kulisoma tangazo katika gazeti la Mambo leo andika barua kwa Mkurugenzi wa kampuni Faidika Limited S.L.P 111 Mwanza ya kuomba nafasi ya kazi S.L.P 100 Mtwara.
- 7. Methali zinafunza na zinaweza kupotosha jamii zisipotumika kwa ukamilifu. Kwa kutumia methali nne, eleza namna kila moja inaweza kupotosha jamii.
- 8. Kwa kuzingatia maumbo ya umoja na wingi tunga sentensi mbili kwa kila ngeli zifuatazo
 - i. YU-A-WA
 - ii. KI-VI
 - iii. I-ZI
 - iv. LI-YA